THE INTERNATIONAL COMMUNION

OF THE

CHARISMATIC EPISCOPAL CHURCH

IBADA YA UBATIZO, KIPAIMARA, KUWAPOKEA WALIOKWISHA KUWEKWA KIPAIMARA KATIKA MAKANISA MENGINE

NA

KUWEKA MASHEMASI NA MAKASISI.

CHARISMATIC EPISCOPAL CHURCH

IBADA YA UBATIZO

KUWALETA NA KUWAPIMA WATAKAOBATIZWA.

Ibada huanza kwa ushirika mtakatifu, baada ya mahubiri, kasisi, au shemasi awakaribishe wanaobatizwa, wazazi, na wadhamini waje mbele ya mahali pa kubatizia.

Kasisi au shemasi aseme:

Wapendwa katika Bwana tumekusanyika mbele za Mungu Mwenyezi Baba wa Mbinguni, ili kushuhudia ubatizo mtakatifu ambao mtu/watu ana/wana batizwa na kuwa kiungo katika mwili wa Kristo ambao ni kanisa. Kwa kazi hii ya sacramenti takatifu iliyoamuriwa na Kristo mwenyewe, mtu/watu huyu/hawa wataifia dhambi na kufufukia katika upya wa maisha kwa kupokea utimilifu wa neema ya Mungu ili wapate kumtumikia yeye katika siku zote za maisha yao AMEN.

Kasisi au askofu awaelekee watu wanaobatizwa, wazazi, na wadhamini na kuwauliza:

MHUDUMU: Je unaomba nini kwenye kanisa takatifu?

WATU: Uzima wa milele katika Kristo Yesu.

KASISI/SHEMASI: Yesu alisema “Na amri ya kwanza ndiyo hii sikia Ee Israeli, Bwana Mungu wetu ni mungu mmoja. Nawe utampenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote. Hii ndiyo amri ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo. Nayo ni hii, “Umpende jirani yako kama nafsi yako” Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi. Je, unazikubali amri hizi?

WATU: Ndivyo nitakavyofanya kwa msaada wa Mungu; na nitatembea katika amri hizi siku zote za maisha yangu.

Kwa wale wasioweza kujibu wenyewe watawakilishwa na wazazi, na wadhamini wao kama ifuatavyo:

WAZAZI/WADHAMINI: Namleta……. Apokee sakramenti ya ubatizo.

Kasisi au askofu awaulize wazazi na wadhamini:

Je, utawajibika kumlea na kumwangalia mtoto huyu ili akue katika imani na maisha ya Kristo?

WAZAZI/WADHAMINI: Ndivyo nitakavyofanya kwa msaada wa Mungu.

MHUDUMU: Je, utajitahidi kwa uwezo wako kumfanya mtoto huyu amfahamu Yesu ili atakapofikia umri wa kuwa na uamuzi wake binafsi wa kumpokea Yesu kuwa mwokozi wake kama unavyoahidi kwa kweli kwa midomo yenu kwa niaba yake?

WAZAZI/WADHAMINI: Ndivyo nitakavyofanya kwa msaada wa Mungu.

MHUDUMU: Je, utawajibika kuona kwamba mtoto unayemleta anajifunza imani ya mitume, sala ya Bwana, Amri kumi, na mambo yote yanayompasa mkristo ayajue na kuyaamini kwa ajili ya kukua kwake kiroho?

WAZAZI/WADHAMINI: Ndivyo nitakavyofanya kwa msaada wa Mungu.

MHUDUMU: Je, utamsaidia mtoto huyu kukua na kufikia kimo cha utimilifu wa Kristo kwa maombi yako, matendo yako na ushuhuda wa maisha yako?

WAZAZI/WADHAMINI: Ndivyo nitakavyofanya kwa msaada wa Mungu.

Kasisi au askofu anyoshe mikono yake kwa wanaobatizwa, wazazi na wadhamini na kusema.

MHUDUMU: Mwenyezi Mungu Baba wa Mbinguni ambaye ameweka nia ndani ya mioyo yenu kuitafuta neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, awajalie nguvu ya Roho Mtakatifu kudumu katika nia hiyo

na kukua katika imani na ufahamu. Kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo.

WATU: Amina.

Kasisi au askofu aweke alama ya msalaba kwa kutumia dole gumba huku akisema:

MHUDUMU: (Fulani) ……. Pokea alama hii ya msalaba katika paji lako la uso na katika moyo wako. Katika Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu.

WATU: Amina.

Mhudumu awaulize watakaobatizwa maswali yafuatayo: ikiwa kama watakaobadtizwa ni watoto wachanga ambao hawawezi kujibu wenyewe, wazazi au wadhamini watajibu kwa niaba yao.

MHUDUMU: Je, unamkataa shetani na kazi zake zote, na majeshi yake yote ya uovu ambayo yanamwasi Mungu?

JIBU: Nayakataa yote.

MHUDUMU: Je, unazikataa nguvu zote mbovu za ulimwengu huu ambazo zinaharibu na kuangamiza viumbe vya Mungu?

JIBU: Nazikataa zote.

MHUDUMU: Je unazikataa tamaa za dhambi na mwili zinazokuvuta utoke katika kumpenda Mungu?

JIBU: Nazikataa zote.

MHUDUMU: Tuombe:

Mwenyezi Mungu uishie milele, ulimtuma mwanao pekee ulimwenguni kuvunja nguvu ya shetani, roho ya uovu ili kumwokoa mwanadamu kutoka katika ufalme wa giza, na kumleta kwenye ufalme wa ajabu wa nuru yako. Tunaomba kwa ajili ya ……. umwondoe kwenye dhambi ya asili umfanye kuwa

hekalu hai la utukufu wako na umtume Roho Mtakatifu akae ndani yake milele, kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

WATU: Amina

Kasisi au askofu ampake mafuta ya ubatizo juu ya kifua na katikati ya bega la kushoto na bega la kulia na kusema.

MHUDUMU: Ninakupaka + mafuta + ya wokovu, katika jina + la Bwana na Mwokozi wetu Kristo anayeishi na kumiliki milele.

Kama hakuna ibada ya kipaimara au ibada ya kuwapokea watu wanaojiunga ila ubatizo tu, ibada ya ubatizo inaendelea.

_____

_____

SAKRAMENTI YA KUWALETA WATU WA KIPAIMARA NA KUWAPOKEA WALE AMBAO WAMEWEKWA KIPAIMARA KATIKA MAKANISA MENGINE.

ASKOFU: Wale wanaowekwa kipaimara waletwe

KASISI: Baba mwenye heshima katika Mungu nakuletea…… kwa sakramenti ya kipaimara takatifu.

(Wale waliowekwa kipaimara na askofu aliye katika mfuatano (hirathi) wa mitume watakaopokelewa katika kanisa la Charismatic Episcopal waletwe sasa)

KASISI: Nawaleta …… ili wapokelewe katika kanisa la Charismatic Episcopal.

Askofu awaulize wale wanaopokelewa:

ASKOFU: Je, mnaahidi kwa kweli kukataa dunia, mwili na shetani?

WANAOPOKELEWA: Nazikataa.

ASKOFU: Je, unajitoa kwa upya kwa Yesu Kristo?

WANAOPOKELEWA: Nitafanya hivyo, na kwa neema ya Mungu nitamfuata yeye kama Bwana na Mwokozi wangu.

Baada ya wote kuletwa askofu awaambie watu kwa kusema:

ASKOFU: Je, ninyi mnaoshuhudia ahadi hizi mtajitahidi kwa uwezo wenu wote kuwasaidia watu hawa wakue katika maisha matakatifu ndani ya Kristo?

WATU: Ndiyo tutakavyofanya kwa msaada wa Mungu.

Kisha askofu atasema maneno haya au maneno yanayofanana na haya.

ASKOFU: Ndugu wapenzi, tuungane na wale wanaojitoa wenyewe sasa kwa Kristo Yesu, nasi tufanye upya ahadi za ubatizo wetu.

AHADI YA UBATIZO.

ASKOFU: Je, unamwamini Mungu Baba?

WATU: Namwamini Mungu Baba Mwenyezi, Muumba Mbingu na nchi.

ASKOFU: Je, unamwamini Yesu Kristo mwana pekee wa Mungu?

WATU: Namwamini Yesu Kristo mwana wake pekee, Bwana wetu aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, akazaliwa na Bikira Mariamu, akateswa zamani za Pontio Pilato, akasulubiwa, akafa, akazikwa, akashuka kuzimu, siku ya tatu akafufuka, akapaa mbinguni, ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi atakuja tena kuwahukumu walio hai na waliokufa.

ASKOFU: Je, unamwamini Mungu Roho Mtakatifu?

WATU: Namwamini Roho Mtakatifu, kanisa takatifu katholiko, ushirika wa watakatifu, ondoleo la dhambi, kufufuliwa kwa mwili, na uzima wa milele.

Watu na wale wanaowekewa kipaimara wanaungana na askofu katika kukiri imani ya mitume.

Hii ndiyo imani yetu. Hii ndiyo imani ya kanisa ambayo tunaona fahari kuikiri katika Kristo Bwana wetu Amina.

ASKOFU: Je, utadumu katika mafundisho ya mitume na ushirika katika kuumega mkate na maombi?

WATU: Ndivyo nitakavyofanya kwa msaada wa Mungu.

ASKOFU: Je, utatangaza kwa maneno na kwa mfano wa maisha yako habari njema za Mungu katika Kristo Yesu?

WATU: Ndivyo nitakavyofanya kwa msaada wa Mungu.

ASKOFU: Je, utatafuta kumtumikia Kristo na watu wote? Kumpenda jirani yako kama nafsi yako?

WATU: Ndivyo nitakavyofanya kwa msaada wa Mungu.

ASKOFU: Je, utajitahidi kutafuta haki na amani miongoni mwa watu wote na kuheshimu utu wa kila mtu?

WATU: Ndivyo nitakavyofanya kwa msaada wa Mungu.

MAOMBI KWA AJILI YA WALE WANAOWEKWA KIPAIMARA.

Ndipo askofu awaambie watu:

ASKOFU: Ndugu wapendwa, Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo alisema, Amin amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuuingia ufalme wa Mungu. Hivyo ninawasihini tumwombe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu awajalie nguvu katika wema wake na rehema zisizo na kikomo awape ..... kile wasichoweza kukipata kwa asili ya ubinadamu ndilo kubatizwa kwa maji na kwa Roho Mtakatifu na kukaribishwa katika kanisa takatifu la Kristo na kufanywa viungo hai vya kanisa. (Na) Jaza Roho wako mtakatifu ndani ya watu hawa ambao wamekwisha kujitoa kwa upya kwa Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao na ambao watathibitishwa na kupokelewa katika sehemu hii ya kanisa la Mungu.

Shemasi aongoze maombi (sala) yafuatayo:

SHEMASI : Uwaokoa ee Bwana kutoka katika njia ya dhambi na mauti.
WATU : Ee, Bwana kwa rehema zako usikie kuomba kwetu.

SHEMASI : Wafungue mioyo yao kwa neema na kweli yako.
WATU : Ee Bwana kwa rehema zako usikie kuomba kwetu.

SHEMASI : Wajaze Roho wako mtakatifu mtoa uzima.
WATU : Ee Bwana kwa rehema zako usikie kuomba kwetu.

SHEMASI : Watunze katika imani na ushirika wa kanisa lako takatifu katholiko.
WATU : Ee Bwana kwa rehema zako usikie kuomba kwetu.

SHAMASI : Wafundishe kupenda na kuwatumikia wengine katika uwezo wa Roho Mtakatifu.
WATU : Ee Bwana kwa rehema zako usikie kuomba kwetu.

SHEMASI : Watume ulimwenguni kuishuhudia Injili yako.
WATU : Ee Bwana kwa rehema zako usikie kuomba kwetu.

SHEMASI : Uwalete katika utimilifu wa amani na utukufu wako.
WATU : Ee Bwana kwa rehema zako usikie kuomba kwetu.

MHUDUMU: Ee Bwana wakirimie wote wanaobatizwa katika mauti ya mwanao Yesu Kristo waweze kuishi katika uwezo wa ufufuo wake na kumtazamia arudi mara ya pili katika utukufu, aishiye na kumiliki sasa hata milele Amina.

WAKATI WA UBATIZO

Kasisi au askofu achukue chumvi kidogo katika vidole vyake na kumwekea kinywani yule anayebatizwa huku akisema.

Pokea roho ya hekima, ikawe ahadi ya uzima wa milele. Amina.

KUBARIKI MAJI.

Kasisi au askofu abariki maji kwanza akisema;

MHUDUMU : Bwana awe nanyi
WATU : Awe pia na roho yako.

MHUDUMU : Inueni mioyo yenu.
WATU : Twaiinua kwa Bwana.

MHUDUMU : Tumshukuru Bwana Mungu wetu.
WATU : Ni haki kumshukuru na kumtukuza.

Mhudumu anaendelea

MHUDUMU: Tunakushukuru mwenyezi Mungu kwa kipawa cha maji ambayo umeifanya kuwa ni ishara ya utajiri wa neema yako unayotupatia katika sakramenti hii. Mwanzo wa uumbaji Roho wako alitulia juu ya maji hayo. Kwa njia ya maji ya gharika ulitupatia ishara ya maji ya ubatizo ambayo hukomesha dhambi na kuleta mwanzo mpya wa wema na rehema. Kwa njia ya maji ya bahari ya shamu uliwaongoza wana wa Israeli toka utumwani Misri hadi kwenye nchi ya ahadi. Katika maji ya mto Yordani mwanao Yesu Kristo alipokea ubatizo wa Yohana na kutiwa mafuta na Roho kama masihi, Kristo kutuongoza kwa njia ya kifo na ufufuo toka utumwa wa dhambi na kuingia katika uzima wa milele.

Tnakushukuru wewe Baba kwa maji ya ubatizo, ndani yake tumezikwa pamoja na Kristo katika mauti yake, kwa ubatizo huo tunashiriki ufufuo wake na tunazaliwa upya na Roho mtakatifu. Kwa hiyo tukiwa tumejaa furaha ya utii wa mwanao ambaye aliwaamuru wanafunzi wake “Enendeni ulimwenguni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu” sasa tunawaleta katika ushirika wake wale wamjiao yeye kwa imani.

Katika maneno yafuatayo mhudumu ayagawe maji huku akifanya alama ya msalaba.

MHUDUMU: Sasa takasa maji haya tunakuomba kwa nguvu ya Roho wako mtakatifu ili huyu/hawa anayetakaswa toka katika

dhambi zote na kuzaliwa upya aweze kudumu milele katika maisha ya Kristo Mwokozi wetu aliyefufuka. Kwa yeye, kwako, na kwa Roho mtakatifu utukufu na heshima viwe vyako sasa na hata milele Amina.

UBATIZO:

MHUDUMU: Mpeni jina mtoto/mtu huyu

Wazazi au wadhamini wataje jina la anayebatizwa mhudumu amzamishe au kumwagia maji yule anayebatizwa mara tatu huku akisema.

MHUDUMU: ……(Fulani) Nakubatiza katika Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Ndipo mhudumu aweke mkono juu ya kichwa cha yule anayebatizwa na kuweka alama ya msalaba katika paji la uso kwa kutumia Krisma Takatifu.

MHUDUMU: Umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu katika ubatizo na kuwekwa alama kuwa mali ya Kristo milele, Amina.

Tunampokea …….(Fulani) katika ushirika wa kundi lake Kristo, tunamtia alama ya msalaba ili kwamba tangu sasa hataona haya kuikiri imani ya Kristo aliyesulubiwa, na akiwa chini ya bendera yake kupigana kwa ushujaa na dhambi na dunia na shetani, na kudumu kuwa askari na mtumishi mwaminifu wa Kristo hata mwisho wa maisha yake Amina.

Kama inahitajika aliyebatizwa anaweza kupewa vazi jeupe huku mhudumu akisema:

MHUDUMU: ……(Fulani) Sasa umefanyika kiumbe kipya na umemvaa Kristo. Pokea vazi hili jeupe kama ishara ya nje ya usafi uliopewa juu yako na alama ambayo kwayo umepaswa kuishi maisha matakatifu ili kwamba baada ya maisha haya yanayopita, uweze kushiriki uzima wa milele Amina.

Mishumaa ya ubatizo inaweza kuwashwa na kupewa yule aliyebatizwa huku mhudumu akisema:

MHUDUMU: Pokea nuru ya Kristo ili kwamba atakapokuja Bwana Arusi uweze kwenda pamoja na watakatifu wote kumlaki, na kuhakikisha kwamba unaitunza neema ya ubatizo wako Amina.

Baada ya tendo hili kumalizika mhudumu akiwa mahali pa kuonekana na watu anyoshe mikono yake juu ya yule aliyebatizwa na kuomba.

MHUDUMU: Tuombe

Baba wa mbinguni tunakushukuru kwamba kwa maji na kwa Roho Mtakatifu umempa……(Fulani) msamaha wa dhambi na umemwinua juu kwenye maisha ya neema. Mfanye adumu Ee Bwana katika Roho wako mtakatifu. Umpe Roho ya utafiti na kupambanua, moyo wa ujasiri, kutaka na kuvumilia, roho ya kujua na kukupenda wewe na kipawa cha furaha na kushangilia kazi zako zote Amina.

Wote wakiisha kubatizwa mhudumu aseme:

MHUDUMU: Tuwapokee waliobatizwa.

MHUDUMU NA WATU: Tunawapokea katika jamii ya nyumba ya Bwana, ikirini imani ya Kristo aliyesulubiwa, tangazeni kufufuka kwake na mshiriki pamoja nasi katika ukuhani wake wa milele.

IBADA YA KIPAIMARA/UTHIBITISHO.

ASKOFU: Wale wanaowekwa mikono waletwe sasa.
KASISI/SHEMASI: Ninakuletea…… kwa sakramenti ya kipaimara

Wanaowekwa mikono wasimame mbele ya Askofu, awaambie yafuatayo.

ASKOFU: Siku ya Pentekoste mitume walipokea Roho Mtakatifu kama alivyoahidi Bwana. Pia walipokea uwezo wa kuwapa wengine Roho Mtakatifu ili kuikamilisha kazi ya ubatizo. Haya tunayasoma katika matendo ya Mitume. Mtume Paulo alipoweka mikono yake kwa wale waliokuwa wamebatizwa, Roho Mtakatifu alikuja juu yao,

na walianza kusema kwa lugha mpya na kwa maneno ya kinabii. Mtakatifu Petro na Mtakatifu Yohana waliwaombea waliobatizwa Samaria wapokee Roho Mtakatifu na udhihirisho wa upako wake ulisababisha furaha kwa wale waliokuwapo. Maaskofu, wakiwa katika mfuatano wa Mitume, wanafuata nyayo zao kuomba ujazo wa Roho Mtakatifu kwa waliobatizwa. Upako wa Roho Mtakatifu mnayempokea utakuwa ishara na mhuri wa kuwafanya mfanane na Kristo na kuwa kiungo safi cha kanisa lake. Alipobatizwa na Yohana, Kristo mwenyewe alijazwa na Roho na kutumwa katika huduma kwa watu, na kuuwasha moto ulimwengu.

Ndipo Askofu anawaambia wanaowekwa mikono maneno haya.

Wapendwa mmezaliwa mara ya pili katika Kristo kwa kubatizwa na mmekuwa viungo vya Kristo na watu na ukuhani wake wa kifalme. Sasa mnashkiriki katika ujazo wa Roho Mtakatifu miongoni mwetu, Roho aliyetumwa na Bwana kwa Mitume siku ya Pentecoste, nao pamoja na waliowafuata waliwapa waliobatizwa.

Nguvu za Roho Mtakatifu zilizoahidiwa ambazo mnazipokea zitawafanya zaidi kuwa kama Kristo, na kuwasaidia kushuhudia juu ya mateso, kifo na kufufuka kwake. Upako wa Roho Mtakatifu utawawezesha kuwa viungo hai vya kanisa, na kwa kutumia vipawa vyenu vya Roho, kuujenga mwili wa Kristo katika imani na upendo.

Kunaweza kukawa na kimya. Kisha Askofu husema:

Mwenyezi Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, kwa maji Roho Mtakatifu uliwaweka huru watoto wako kutoka dhambi na kuwapa maisha mapya katika Kristo. Mtume Roho wako Mtakatifu juu ya ..... kuwa msaidizi wake na kiongozi. Mpe roho ya hekima na ufahamu, roho wa shauri na nguvu za rohoni, roho wa maarifa na utauwa; mjaze na roho ya kicho chako kitakatifu. Tunaomba haya kwa njia ya Kristo Bwana wetu.

Wanaowekwa kipaimara wasimame, na Askofu awanyoshee mikono yake aseme nao wakijibu.

ASKOFU : Pokea Roho wa Hekima.
JIBU : Amin

ASKOFU : Pokea Roho wa Ufahamu
JIBU : Amin

ASKOFU : Pokea Roho wa Ushauri.
JIBU : Amin

ASKOFU : Pokea Roho wa Nguvu za Rohoni.
JIBU : Amin

ASKOFU : Pokea Roho wa Maarifa.
JIBU : Amin

ASKOFU : Pokea Roho wa kweli wa kiungu.
JIBU : Amin

ASKOFU : Wajaze Roho wa kicho sasa na hata milele.
JIBU : Amin.
ASKOFU : Na Tuombe
Ee Bwana, umlinde mtumishi wako huyu, kwa neema yako ya mbinguni, adumu kuwa wako milele, naye azidi kukua kila siku katika Roho wako Mtakatifu, hata aufikie ufalme wako wa milele.

JIBU: Amin.

Anayewekwa mikono apige magoti mbele ya Askofu ambaye hufanya ishara ya msalaba kwa Karisma Takatifu penye paji la uso akisema:

ASKOFU: Pokea mhuri wa kipawa cha Roho Mtakatifu.

Kisha Askofu ataweka mikono juu ya mmoja akisema:

ASKOFU: Ee Bwana mtie nguvu mtumishi wako……. kwa Roho wako mtakatifu, mwezeshe kwa huduma yako, na mtegemeze siku zote za maisha yake. Ameni.

ASKOFU: Ninakutia alama ya msalaba + na kukuthibitisha kwa mafuta ya furaha, katika jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amen.

Askofu hupapasa shavu la mwekwa kipaimara na kusema kumbuka Yesu alisema kwamba, “Ulimwenguni mnayo dhiki, lakini jipeni moyo, mimi nimeushinda ulimwengu” yohana 16:33.

==========KWA MAPOKEZI==========

Kila aliyewekwa kipaimara na anayepokelewa atapiga magoti na Askofu amwendee kila mmoja, huku akifanya alama ya msalaba akitumia Krisma Takatifu na kusema:

ASKOFU: Tunakutambua wewe kama kiungo cha kanisa moja takatifu katoliko na Apostoliko, na tunakupokea katika International Communion of the Charismatic Episcopal Church (Ushirika wa Kimataifa wa CEC). Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu Akubariki, akuhifadhi na kukutuma. Pokea kwa upya upako wa Roho Mtakatifu kukuwezesha katika huduma kwa Mungu na Kanisa lake.

Kisha Askofu anyoshe mikono juu ya waliothibitishwa na waliopokelewa akiomba:
Mwenyezi Mungu uishiye milele achilia mkono wako wa ubaba uwe juu ya hawa watumishi wako daima na Roho wako Mtakatifu awe nao daima, na pia waongoze katika maarifa na utii wa neno lako, ili kwamba waweze kukutumikia wewe katika ulimwengu huu, na kuishi na wewe katika maisha yajayo – Kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amen.

Watu wanaweza kupeana amani

MHUDUMU: Amani ya Bwana ikae nanyi daima.
WATU: Ikae na Roho yako.

Ibada ya ushirika mtakatifu iendelee, kwa kutoa kwanza matoleo.

USHIRIKA MTAKATIFU

Ibada ya kuweka Shemasi na Kasisi

Liturgia kwa ajili ya kutangaza neno la Mungu, kuweka wakfu shemasi, na kuadhimisha ushirika mtakatifu.

Mwanzo
Wimbo wa kuingia
Sifa na shangwe.

ASKOFU: Kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.
WATU: Amina

ASKOFU: Nitakwenda madhabahuni pa Mungu.
WATU: Kwa Mungu aipaye nafsi yangu furaha.

ASKOFU: Msaada wetu + u katika jina la Bwana
WATU : Aliyeziumba mbingu na nchi

ASKOFU : Bwana awe nanyi.
WATU : Awe pia nawe.

Wote wapige magoti ndipo askofu aseme sala ya utakaso:

Mwenyezi Mungu ambaye kwako mioyo yote i wazi haja zote hujulikana, na kwako hakuna siri iliyofichika: Utakase mawazo ya mioyo yetu kwa uwezo wa Roho wako Mtakatifu, ili tukupende kwa kweli na kuliinua kwa uthamani Jina lako Takatifu kwa Kristo Bwana wetu. Amina.

Shemasi aseme amri kuu:

Yesu alisema, “Amri ya kwanza ni hii: sikia, Ee Israeli Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja. Umpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote. Na ya pili ni hii. Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi.” Mk 12:29-30.

Shemasi awaalike watu wajipeleleze dhambi zao na kuzitubu kimya kimya.

Ndugu zangu, tunapojianda kusherehekea siri ya Upendo wa Kristo, tumuungamie Mungu dhambi zetu ili tupate kusamehewa na kutiwa nguvu.

Wote wakae kimya kwa muda. Halafu huku wakiongozwa na shemasi wote waseme.

Mungu mwenye rehema nyingi tunaungama kwamba tumekutenda dhambi kwa mawazo, maneno, na matendo, kwa yale tuliyofanya na kwa yale ambayo tumeacha kuyafanya. Tumeacha kukupenda kwa mioyo yetu yote; tumeacha kuwapenda majirani zetu kama nafsi zetu. Tunasikitika kwa kweli na kwa unyenyekevu tunatubu. Kwa ajili ya mwana wako Yesu Kristo, tuhurumie na utusamehe; ili tuweze kufurahia katika mapenzi yako, na kuenenda katika njia zako, kwa utukufu wa jina lako. Amina.

Askofu asimame na kusema:

Mwenyezi Mungu aturehemu, tusamehe dhambi zetu, na utulete kwenye uzima wa milele. Amina.

Askofu atoe ghofira:

Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye ameliachia kanisa lake uwezo wa kusamehe wenye dhambi watubuo kwa kweli na kumwamini yeye kwa rehema zake kuu, akusameheni dhambi zetu zote; na kwa mamlaka niliyopewa, ninawatangazieni msamaha wa dhambi zenu zote kwa Jina la + Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Amina.

Sifa na kuabudu.

Wote wasimame

Utukufu una Mungu juu mbinguni, na amani duniani, kwa watu aliowaridhia. Twakusifu, twakuhimidi, twakuabudu, twakutukuza, twakushukuru. Kwa ajili ya utukufu wako Mkuu, Bwana Mungu, mfalme wa mbinguni Mungu baba Mwenyezi. Ee Bwana, Mwana pekee, Yesu Kristo; Bwana Mungu, Mwana kondoo wa Mungu, mwana wa Baba uchukuaye dhambi za ulimwengu, uturehemu, uichukuaye dhambi za ulimwengu, ukubali ukubali kuomba kwetu. Uketiye mkono wa kuume wa Mungu Baba, uturehemu.

Kwa kuwa ndiwe peke yako mtakatifu; ndiwe peke yako Bwana, ndiwe peke yako uliye juu, Yesu Kristo, pamoja na Roho Mtakatifu, katika utukufu wa Mungu Baba. Amina.

Nyimbo za sifa na kuabudu

(Tafadhari msikilize Roho Mtakatifu kufunua karama za lugha, unabii, tafsiri za lugha na kuabudu katika Roho)

Sala ya kuweka wakfu
ASKOFU : Bwana awe nanyi.
WATU : Awe pia nawe.
ASKOFU : Na Tuombe.

Wote wapige magoti.

Baba wa mbinguni, umewafundisha watumishi wa kanisa lako kwamba wasitamani kutumikiwa, bali wawatumikie ndugu zao katika kazi zao na wadumu katika maombi yao, wakitenda huduma zao kwa unyenyekevu na kuwajali wengine. Tunaomba hivi katika Yesu Kristo Bwana wetu, aishiye na kumiliki pamoja nawe katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu mmoja, sasa na hata milele. Amina.

Wote wakae
Somo la kwanza Hesabu 3:5-10a

Zaburi Zaburi 96:

Katika aya ya mwisho wa zaburi, wote wasimame.

Utukufu una Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, ulivyokuwa mwanzo, ulivyo sasa na hata milele ni vivyo. Amina.

Wote wakae
Somo la pili Matendo 6:1-7a

Wote wasimame
Wimbo

Injili takatifu Mathayo 20:25-28

Injili inapotangazwa kabla injili haijasomwa watu waitikie:
“Utukufu ni kwako Bwana Yesu Kristo”

Baada ya Injili kusomwa waitikie

Sifa ni kwako, Bwana Yesu Kristo”

Watu wakae kwa ajili ya hotuba.

Hotuba

Wote wasimame na kusema.
Imani ya Nikea
Kusema kwa pamoja:
(Ni vyema kuinama kabisa wakati vipengele vilivyopigiwa mistari vinaposemwa).

Tunamwamini Mungu mmoja, Baba, Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi, na vitu vyote, vinavyoonekana na visivyoonekana.

Tunamwamini Bwana mmoja, Yesu Kristo, mwana pekee wa Mungu, mwana wa azali wa Baba, yu Mungu kutoka katika Mungu, Nuru kutoka katika Nuru, yu Mungu kweli kutoka katika Mungu kweli, mwana wa azali asiyeumbwa, Mwenye uungu mmoja na Baba. Kwa yeye vitu vyote viliumbwa.

Aliyeshuka kutoka mbinguni kwa ajili yetu wanadamu
na kwa wokovu wetu: Akatwaa mwili kwa uwezo wa Roho Mtakatifu katika Bikira Mariamu, akawa mwanadamu. Akasulubiwa kwa ajili yetu zamani za Pontio Pilato, aliteswa akafa, akazikwa. Siku ya tatu akafufuka kama yanenavyo maandiko matakatifu, akapaa mbinguni ameketi mkono wa kuume wa Baba. Naye atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio hai na wafu, na ufalme wake hautakuwa na mwisho.

Twamwamini Roho Mtakatifu Bwana mtoa uzima atokaye katika Baba na Mwana anayeabudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, aliyenena kwa vinywa vya manabii; Twaamini kanisa moja takatifu katholiko na apostoliko, tunakiri ubatizo mmoja wa kuondolea dhambi, twatazamia kufufuliwa kwa wafu, na uzima wa ulimwengu ujao. Amina.

Baada ya imani ya Nikea, Askofu, huku akiwa amevaa kofia yake ya kiaskofu, aketi katika kiti chake na watu wote wakae.

KUMWEKA WAKFU SHEMASI

Kuitwa na kuletwa anayewekwa ushemasi.

Archdikoni amwite yule anayewekwa katika daraja ya ushemasi.

……, anayewekwa ushemasi, tafadhari apite mbele
Naye ajibu "Nipo"
Na aende kwa askofu, mbele yake ambaye anafanya ishara ya heshima.

Kasisi na mlei, na baadhi ya watu waliopo kama itahitajika wasimame pembeni ya anayewekwa na mbele ya askofu, na kumleta kila anayewekwa, kwa kusema.

WANAOMLETA: ……, Askofu katika kanisa la Mungu, kwa niaba ya wachungaji na watu wa ……, tunamleta kwako…… afanywe kuwa shemasi katika kanisa la Kristo takatifu katholiko.

ASKOFU: Je amechaguliwa kutokana na kanuni za kanisa hili? Na je, mnaamini mwenendo wa maisha yake unafaa katika huduma hii?

WANAOMLETA: Tunathibitisha mbele yako kwamba ametimiza matakwa ya kanuni, na tunaamini anafaa kwa daraja hili.

Askofu awaambie wanaowekwa:
Je, mtakuwa waaminifu kwa mafundisho, marudi na ibada ya Kristo kama kanisa hili lilivyoyapokea?
Na kutokana na kanuni za kanisa hili utamtii askofu wako na watumishi wengine watakaokuwa na mamlaka juu yako na juu ya huduma yako?

Wote wanaowekwa wajibu kwa pamoja:
Ninakubali na niko tayari kufanya hivyo, na kwa moyo wote natamka kwamba nayaamini maandiko matakatifu ya agano la kale na ya agano jipya kuwa ni neno la Mungu, na kuwa na mambo yote ya faradhi kwa wokovu; na kwa moyo wote, ninaahidi kufuata mafundisho, marudi, na ibada ya kanisa la Charismatic Episcopal.

Anayewekwa ushemasi aweke sahihi ya tamko hili hapa juu mbele ya watu wote waliopo.
Baada ya kumaliza kuweka sahihi, anayewekwa arudi na kusimama mbele ya askofu, waliomleta wakae.

Watu sasa wanaweza kusimama huku askofu akiwa ameketi awaambie.

Wapendwa wangu katika Kristo, mnajua umuhimu wa huduma hizi, na uzito wa wajibu wenu katika kumleta .....awekwe mikono katika daraja takatifu la ushemasi. Ikiwa kuna mtu miongoni mwenu ajuaje zuio lolote au hatia yoyote inayozuia tusimwingize katika huduma hii, aje mbele sasa na aonyeshe ni hatia gani.

Kama hakuna zuio lolote asikofu aendelee kwa kuuliza:

ASKOFU: Je, mnakubali kwamba ..... awekwe kuwa shemasi?
WATU: Ndiyo.

ASKOFU : Je, mtamtegemeza mtu huyu katika huduma yake?
WATU : Ndivyo tutakavyofanya.

Mausia

Watu wakiwa wamekaa. Askofu awaelekee wanaowekwa kuwa mashemasi, huku wakiwa wamesimama mbele yake.

Mwanangu, umeinuliwa kuwa katika daraja la mashemasi. Bwana amekuwekea kielelezo cha kufuata. Ukiwa shemasi utamtumikia Yesu Kkristo ambaye alijulikana kwa wanafunzi wake kama yule atumikiaye wengine. Fanya mapenzi ya Mungu kwa ukarimu. Mtumikie Mungu na watu kwa upendo na furaha, uuone uasherati na tamaa ya mali kama ibada ya miungu ya uongo; kwa kuwa hakuna mtu awezaye kuwatumikia mabwana wawili. Kama vile mitume walivyochagua watu kwa ajili ya kazi ya huruma, yakupasa uwe mtu mwenye sifa njema, uliyejaa hekima na Roho Mtakatifu. Jionyeshe mbele ya Mungu na watu kwamba u-mtu asiyelaumika,

mtumishi halali wa Kristo na wa siri za Mungu, mtu aliyeimarika katika imani.

Kamwe usigeuke na kuliacha tumaini ambalo umelipata katika Injili, haikupasi kulisikia neno la Mungu tu, bali ulihubiri pia. Shikilia siri ya imani kwa dhamiri safi. Onyesha kwa matendo neno unalolihubiri kwa kinywa chako.

Ndipo watu wa Kristo, waletwe na Roho kwenye uzima, watakuwa sadaka inayokubalika kwa Mungu. Hatimaye siku ya mwisho, utakapokutana na Bwana, utamsikia akisema; “Vema, Mtumwa mwema na mwaminifu, ingia katika furaha ya Bwana wako”.

Anayewekwa ajibu:
Amina.

Kutahini: **Shemasi**

Askofu awaulize wanaowekwa katika daraja ya ushemasi.

Mwanangu, kabla hujawekwa kuwa shemasi, yakupasa ukiri mbele ya watu nia yako katika kuingia katika daraja hii.

Je, unakubali kuwekwa katika huduma ya kanisa kwa kuwekewa mikono na karama ya Roho Mtakatifu?

Anayewekwa ajibu: Ninakubali.

ASKOFU : Je, unakusudia kutoa huduma ya ushemasi kwa unyenyekevu na upendo katika kumsaidia askofu na makasisi na kuwatumikia watu wa Kristo?

ANAYEWEKWA : Ndiyo.

ASKOFU : Je, unakusudia kuishika siri ya imani kwa dhamiri safi, kama mtume anavyosihi, na kuitangaza imani hii kwa maneno na matendo kama inavyofundishwa katika Injili na mapokeo ya kanisa?

ANAYEWEKWA : Ndiyo.

ASKOFU : Je, unakusudia kushika na kuendeleza kwa kina roho ya maombi ifaayo katika mwenendo wa maisha yako na kutunza kile unachotakiwa, kuadhimisha kwa uaminifu huduma ya kila siku kwa kanisa na kwa ulimwengu wote?

ANAYEWEKWA: Ndiyo.

ASKOFU : Je, unakusudia kutengeneza maisha yako (na yale ya familia yako au nyumba yako au jamii) kila mara kufuatana na kielelezo cha Kristo ambaye mwili wake na damu yake utawapa watu?

ANAYEWEKWA : Ndiyo.

ASKOFU : Je, unakusudia kuwa mwaminifu katika kusoma na kujifunza maandiko matakatifu?

ANAYEWEKWA : Ndiyo.

ASKOFU : Bwana ambaye amekupa nia ya kutenda mambo haya akupe neema na uwezo wa kuyatenda.

ANAYEWEKWA: Amina.

Ahadi ya Utii.

Anayewekwa aende kwa askofu na kupiga magoti mbele yake na aweke mikono yake miwili katikati ya mikono ya askofu.

ASKOFU : Je, unaahidi kuniheshimu na kunitii na wale watakaonifuata?
ANAYEWEKWA : Ndiyo, naahidi.

ASKOFU: Mungu aliyeanzisha kazi njema ndani yako aikamilishe.

KUWEKA WAKFU MAKASISI

Askofu, huku akiwa amevaa kofia yake, akae kitini pake, watu wote wanaweza kukaa.

Kuwaita na kuwaleta wanaowekwa ukasisi.

Wanaowekwa katika daraja takatifu la Ukasisi wanaitwa na Mkuu wa Sherehe (master of ceremonies).

.....Wale wanaokwenda kuwekwa Makasisi, njoni mbele tafadhali.

WAJIBU:
"Tupo"
na waende kwa askofu, wapige magoti, halafu wasimame kwa kujipanga mbele yake.

Wanaowaleta, angalau kasisi mmoja na mlei mmoja kwa kila anayewekwa, wanaowaleta wanaweza kuongezwa kama inahitajika, waje wasimame kando ya wanaowekwa na mbele ya askofu.

Kuwaleta : Makasisi.

Wanaowekwa waletwe kwa kuungana na wadhamini wao.

WANAOWALETA:....., Askofu katika kanisa la Mungu, kwa niaba ya wachungaji na watu wa kansia la Charismatic Episcopal la ..... tunawaleta kwako.....waamuriwe kuwa makasisi katika kanisa takatifu la Kristo, Katholiko.

ASKOFU : Je, wamechaguliwa kutokana na kanuni za kanisa hili? Na je, mnaamini mwenendo wa maisha yao unafaa katika kufanya huduma hii?

WANAOWALETA : Tunathibitisha kwako kwamba wametosheleza matakwa ya kanuni (Canons) na tunaamini wanastahili kwa daraja hili.

Nadhiri Takatifu.

Askofu awaelekee wote wanaowekwa:

Je, mtakuwa waaminifu katika mafundisho, marudi, na ibada ya Kristo kama ambavyo kanisa hili limeyapokea? Na kutokana na kanuni za kanisa hili, mtamtii askofu wenu na watumishi wengine watakaokuwa na mamlaka juu yenu na kazi yenu?

Wanaowekwa wajibu kwa pamoja.
Ninakubali na niko tayari kufanya hivyo; na kwa moyo wote natamka kwamba nayaamini maandiko matakatifu ya Agano la kale na ya Agano Jipya kuwa neno la Mungu na kuwa na mambo yote ya faradhi kwa wokovu; na kwa moyo wote naahidi kufuata mafundisho, marudi, na ibada ya The International Communion of the Charismatic Episcopal Church.

Ndipo wale wanaowekwa ukasisi waweke sahihi zao katika nadhiri zao takatifu mbele ya watu wote waliopo. Halafu Canon Missioners au watu walioteuliwa, na askofu akishuhudia sahihi zao. Watu wote wanaweza kuwa wamesimama huku wakiimba wakati wa kutia sahihi. Waliowaleta warudi kwenye viti vyao.

Baada ya wote kuweka sahihi, wanaowekwa warudi na kuja kusimama mbele ya askofu, watu wengine waendelee kusimama.

Askofu akiwa amekaa kwenye kiti chake awaambie watu:
Ndugu zangu wapendwa katika Kristo, mnajua umuhimu wa huduma hizi, na uzito wa wajibu wenu katika kuwaleta..... Waamuriwe katika daraja takatifu la Ukasisi. Hivyo kama kuna mtu miongoni mwenu ajuaye zuio au hatia yoyote inayomzuia tusimwingize katika huduma hii aje mbele sasa na aonyeshe ni hatia gani.

Iwapo hakuna zuio lolote, askofu aendelee kuwauliza watu juu ya kila atakayewekwa.

ASKOFU : Je, ni mapenzi yenu kwamba ..... awekwe kuwa Kasisi?
WATU : Ndiyo.

ASKOFU : Je, Mtawategemeza watu hawa katika huduma zao?
WATU : Ndiyo.

Wote wakae.

Mausia : Makasisi.

Askofu awaambie wale watakaowekwa ukasisi ambao watakuwa wamesimama mbele maneno haya:

Wanangu, mmeinuliwa sasa katika daraja la ukasisi. Yawapaseni kutumia uwezo wenu katika wajibu wa kufundisha katika jina la Kristo, mwalimu Mkuu. Shirikisheni neno la Mungu kwa watu ambalo umelipokea kwa furaha. Itafakarini sheria ya Mungu, myaamini yale myasomayo, myafundishe yale mnayoyaamini, na yatendeeni kazi yale mnayoyafundisha.

Mafundisho mnayofundisha yaweze kuwa chakula kwa watu wa Mungu. Maisha yenu yakawe mfano yakawavute wafuasi wa Kristo, ili kwamba kwa maneno na matendo yenu muweze kuijenga nyumba ambayo ni kanisa la Mungu.

Kwa njia hiyo hiyo yawapaseni kuubeba utume wenu wa kutakasa katika uwezo wa Kristo. Huduma yenu itakamilisha dhabihu ya kiroho ya waaminifu kwa kuiunganisha na ile ya Kristo, dhabihu inayotolewa ki-sacramenti katika mikono yenu. Fahamuni kile mnachokifanya na muige siri mnayoiadhimisha katika kukumbuka mauti ya Bwana na ufufuo, jitahidini kuwa wafu katika dhambi na kutembea katika upya wa maisha ya Kristo.

Mtakapobatiza, mtawaleta watu wote katika kuwa watu wa Mungu. Katika sakramenti ya toba mtasamehe dhambi katika jina la kristo na kanisa. Kwa kutumia mafuta mtaponya na kufariji wagonjwa. Mtaadhimisha (celebrate) liturgia na kutoa shukrani na sifa kwa Mungu kila siku, kwa kuwaombea si watu wa Mungu tu, bali kwa ulimwengu wote. Kumbukeni kwamba mmechaguliwa toka miongoni mwa watu wa Mungu na kuwekwa kutenda kwa ajili yao katika kuhusiana na Mungu. Fanyeni sehemu yenu katika kazi ya

Kristo, Kasisi mwenye furaha na upendo wa kweli, tumikia mambo yamhusuyo Kristo kabla ya yale yakuhusuyo wewe.

Hatimaye kumbukeni kushiriki katika kazi ya Kristo, aliye kichwa na mchungaji wa kanisa, na mkiungana na askofu na kumtii, tafuteni kuwaleta waaminifu pamoja kwenye jamii moja na kuwaongoza vyema, kwa njia ya Kristo na katika Roho wake mtakatifu, kwa Mungu Baba. Daima kumbukeni kielelezo cha mchungaji mwema ambaye alikuja kutumika si kutumikiwa, na kutafuta na kuokoa waliopotea..

Kutahini : Makasisi

Ndipo askofu awaulize kwa pamoja wale wanaowekwa:

ASKOFU : Wanangu, kabla hamjaendelea kwenye daraja ya ukasisi yawapaseni kutamka mbele ya watu nia yenu ya kuingia katika daraja hii ya ukasisi.

Je, mnakusudia, kwa msaada wa Roho Mtakatifu; kutoa huduma pasipo kuchoka katika daraja ya ukasisi kama watenda kazi wenye bidii pamoja na maasikofu katika kulitunza kundi la Bwana?

ANAYEWEKWA : Ndiyo.

ASKOFU : Je, mnakususia kusherehekea siri za Kristo kwa uaminifu na kwa kidini kama kanisa lilivyotukabidhi, kwa utukufu wa Mungu na kuwatakasa watu wa Kristo?

WANAOWEKWA : Ndiyo.

ASKOFU : Je, mnakusudia kutenda huduma ya neno istahilivyo na kwa hekima, mkiihubiri injili na kuielezea imani katholiko?

WANAOWEKWA: Ndiyo.

ASKOFU : Je, mnakusudia kuwa na bidii katika kusoma na kujifunza maandiko matakatifu, na katika kutafuta maarifa ya

mambo yale yanayowafanya muwe imara na wahudumu wa Kristo wenye uwezo zaidi?

WANAOWEKWA : Ndiyo.

ASKOFU : Je, mnakusudia maisha yenu na ya familia zenu kuwa kielelezo kinachofanana na mafundisho ya Kristo ili kwamba muwe kielelezo safi kwa watu wenu?

WANAOWEKWA : Ndiyo.

ASKOFU : Je, mnakusudia kudumu katika maombi ya watu wote, na ya binafsi, mkiomba neema ya Mungu kwa ajili yenu wenyewe na kwa ajili ya watu wengine, mkimpa Mungu kazi zenu zote, kupitia maombezi ya Yesu Kristo, na katika utakaso wa Roho Mtakatifu?

WANAOWEKWA: Ndiyo.

ASKOFU : Je, mnakusudia kuyaweka wakfu maisha yenu kwa Mungu kwa ajili ya wokovu wa watu wake, na kuunganishwa kila siku kwa karibu zaidi na Kristo ambaye ni kuhani Mkuu; aliyejitoa mwenyewe kwa ajili yetu kwa Baba kama dhabihu kamilifu?

WANAOWEKWA : Ndiyo, kwa msaada wa Mungu.

ASKOFU : Mungu aliyekupa nia ya kufanya mambo haya akupe neema na uwezo kuyatenda haya.

WANAOWEKWA : Amina.

Ahadi ya Utii: Makasisi

Kila anayewekwa aende na kupiga matoti mbele ya askofu kwa zamu, na kuweka mikono yake yote katikati ya mikono ya askofu.

ASKOFU : Je, unaahidi kuniheshimu na kunitii na wale watakaonifuata?

ANAYEWEKWA : Naahidi.

ASKOFU : Mungu aliyeanzisha kazi njema ndani yako aikamilishe.

ANAYEWEKWA : Amina.

Litania

Ndipo wote wasimame na askofu, huku akiwa amevua kofia yake, awaalike watu kuomba.

Ndugu zangu wapendwa, tuombe kwamba Baba mwenye nguvu zote amimine karama za mbinguni juu ya mtumishi wake huyu ambaye amemchagua kuwa shemasi.

Shemasi (isipokuwa wakati wa pasaka).

Na tupige magoti.

Anayewekwa alale kifudifudi. Shemasi au mtu aliyechaguliwa awaongoze watu kusema Litania ya kuwekwa mikono.

Kwa amani tuombe kwa Bwana.
Kyrie Eleison, au Bwana uturehemu.
Kyrie Eleison. Au Bwana uturehemu.

Christe Eleison. Au Kristo uturehemu
Christe Eleison. Au Kristo uturehemu.

Kyrie Eleison. Au Bwana uturehemu
Kyrie Eleison. Au Bwana uturehemu.

Mungu Baba
Uturehemu

Mungu Roho Mtakatifu
Uturehemu

Utatu Mtakatifu, Mungu mmoja

Uturehemu

Tunaomba kwako, Bwana Kristo
Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya kanisa takatifu la Mungu, ili liweze kujazwa na kweli na upendo, na lisionekane kuwa na hatia siku ya kuja kwako, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya watu wote wa kanisa lako katika wito na huduma zao, kwamba wakutumie wewe kwa kweli na maisha ya utauwa, Twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya ..... Patriarch wetu kwa ajili ya ..... askofu wetu mkuu, kwa ajili ya ..... askofu wetu na kwa ajili ya maaskofu wote, makasisi na mashemasi, ili kwamba waweze kujazwa na upendo wako, waweze kuwa na njaa ya kweli, na waweze kuwa na kiu ya haki, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Askofu aendelee kuwaombea wanaowekwa wakfu wakiwa na familia zao.

Kwa ajili ya ..... Aliyechaguliwa (Shemasi au Kasisi), katika kanisa lako takatifu katholiko, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwamba kwa uaminifu aweze kutimiza wajibu wake katika huduma hii, alijenge kanisa lako, na kulitukuza jina lako, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwamba kwa kukaliwa na Roho Mtakatifu aweze kudumishwa na kutiwa moyo kuvumilia hadi mwisho, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya familia yake, waweze kupambwa na wema wote wa Kikristo, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Msomaji wa Litania aendelee:

Kwa wote wanaomcha Mungu na kukuamini wewe Bwana Kristo, kwamba migawanyiko yetu ipate kukoma na ya kwamba wote tuwe wamoja kama wewe na Baba mlivyo na umoja, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya utume wa kanisa, kwamba kwa kushuhudia kwa uaminifu liweze kuhubiri injili ulimwenguni kote, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya wale ambao bado hawajaamini, na kwa ajili ya wale waliopoteza imani yao, ili waweze kupokea nuru ya Injili, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya amani ya dunia, ili kwamba roho ya heshima na uvumilivu iweze kukua miongoni mwa mataifa na watu, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya watawala hasa ……. Rais wetu; na wengine wote walio na mamlaka katika nchi yetu, ili waweze kutumika kwa haki na kuinua heshima na uhuru wa kila mtu, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya wale waliofariki katika ushirika wa kanisa lako, na wale ambao imani yao inajulikana kwako peke yako, kwamba, pamoja na watakatifu wote, wapate kupumzika mahali ambapo hakuna maumivu au majonzi, bali uzima wa milele, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya kufurahia ushirika wa watakatifu wote, na tujikabidhi wenyewe, na kila mtu kwa mwenzake, na maisha yetu yote kwa Kristo Mungu wetu.

Kwako, Ee Bwana Mungu wetu.
==========
[*following petition should be inserted here in lieu of above]*
"Tukiufurahia ushirika wa bikira Maria mbarikiwa, pamoja na watakatifu wote, na tukabidhi maisha yetu na maisha yaw engine kwa Kristo aliye Bwana na Mungu wetu"

Kwako ee Bwana Mungu wetu
==========
Yesu Mwana wa Mungu aliye hai,
Bwana usikie kuomba kwetu.

Kristo, utusikie,
Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu,
Kristo uturehemu.
Bwana, uturehemu,

Bwana awe nanyi.
Awe pia nawe,

Na tuombe.

Askofu asimame na kusema,
Bwana Mungu wetu sikia dua zetu, na utupe msaada katika tendo hili la huduma. Tunaona mtu huyu anastahili kutumika kama

shemasi na tunakuomba umbariki na kumtakasa. Utupe haya kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu.

Amina

Litania

Ndipo wote wasimame na askofu, huku akiwa amevua kofia yake, awaalike watu kuomba.

Ndugu zangu wapendwa, tuombe kwamba Baba mwenye nguvu zote amimine karama za mbinguni juu ya mtumishi wake huyu ambaye amemchagua kuwa shemasi.

Shemasi (isipokuwa wakati wa pasaka).

Na tupige magoti.

Anayewekwa alale kifudifudi. Shemasi au mtu aliyechaguliwa awaongoze watu kusema Litania ya kuwekwa mikono.

Kwa amani tuombe kwa Bwana.
Kyrie Eleison, au Bwana uturehemu.
Kyrie Eleison. Au Bwana uturehemu.

Christe Eleison. Au Kristo uturehemu
Christe Eleison. Au Kristo uturehemu.

Kyrie Eleison. Au Bwana uturehemu
Kyrie Eleison. Au Bwana uturehemu.

Mungu Baba
Uturehemu

Mungu Roho Mtakatifu
Uturehemu

Utatu Mtakatifu, Mungu mmoja
Uturehemu

Tunaomba kwako, Bwana Kristo
Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya kanisa takatifu la Mungu, ili liweze kujazwa na kweli na upendo, na lisionekane kuwa na hatia siku ya kuja kwako, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya watu wote wa kanisa lako katika wito na huduma zao, kwamba wakutumie wewe kwa kweli na maisha ya utauwa, Twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya ..... Patriarch wetu kwa ajili ya ..... askofu wetu mkuu, kwa ajili ya ..... askofu wetu na kwa ajili ya maaskofu wote, makasisi na mashemasi, ili kwamba waweze kujazwa na upendo wako, waweze kuwa na njaa ya kweli, na waweze kuwa na kiu ya haki, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Askofu aendelee kuwaombea wanaowekwa wakfu wakiwa na familia zao.

Kwa ajili ya ..... Aliyechaguliwa (Shemasi au Kasisi), katika kanisa lako takatifu katholiko, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwamba kwa uaminifu aweze kutimiza wajibu wake katika huduma hii, alijenge kanisa lako, na kulitukuza jina lako, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwamba kwa kukaliwa na Roho Mtakatifu aweze kudumishwa na kutiwa moyo kuvumilia hadi mwisho, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya familia yake, waweze kupambwa na wema wote wa Kikristo, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Msomaji wa Litania aendelee:

Kwa wote wanaomcha Mungu na kukuamini wewe Bwana Kristo, kwamba migawanyiko yetu ipate kukoma na ya kwamba wote tuwe wamoja kama wewe na Baba mlivyo na umoja, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya utume wa kanisa, kwamba kwa kushuhudia kwa uaminifu liweze kuhubiri injili ulimwenguni kote, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya wale ambao bado hawajaamini, na kwa ajili ya wale waliopoteza imani yao, ili waweze kupokea nuru ya Injili, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya amani ya dunia, ili kwamba roho ya heshima na uvumilivu iweze kukua miongoni mwa mataifa na watu, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya watawala hasa ……. Rais wetu; na wengine wote walio na mamlaka katika nchi yetu, ili waweze kutumika kwa haki

na kuinua heshima na uhuru wa kila mtu, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya wale waliofariki katika ushirika wa kanisa lako, na wale ambao imani yao inajulikana kwako peke yako, kwamba, pamoja na watakatifu wote, wapate kupumzika mahali ambapo hakuna maumivu au majonzi, bali uzima wa milele, twaomba kwako Ee Bwana.

Bwana, usikie kuomba kwetu.

Kwa ajili ya kufurahia ushirika wa watakatifu wote, na tujikabidhi wenyewe, na kila mtu kwa mwenzake, na maisha yetu yote kwa Kristo Mungu wetu.

Kwako, Ee Bwana Mungu wetu.

Yesu Mwana wa Mungu aliye hai,
Bwana usikie kuomba kwetu.

Kristo, utusikie,
Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu,
Kristo uturehemu.
Bwana, uturehemu,

Bwana awe nanyi.
Awe pia nawe,

Na tuombe.

Askofu asimame na kusema,
Bwana Mungu wetu sikia dua zetu, na utupe msaada katika tendo hili la huduma. Tunaona mtu huyu anastahili kutumika kama shemasi na tunakuomba umbariki na kumtakasa. Utupe haya kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu.

Amina

Wote wasimame isipokuwa wanaowekwa wabaki kifudifudi huku wimbo ufuatao ukiimbwa. Askofu avae kofia yake hadi ibada hii itakapomalizika.

MUUMBA ROHO UTUJIE

Muumba Roho, utujie,
Ukae mioyoni mwetu,
Umeziumba roho zetu,
Zijaze neema ya mbinguni.

Waitwa nasi Mfariji,
Karama yake Mtukufu,
Chemi Chemi ya Uhai, moto,
Mafuta ya rohoni, Pendo.

Karama saba utoaye,
Kidole chake Mungu Baba,
Ahadi yake Baba, wewe
Wa kunenesha ndimi zetu.

Kipindi cha Ukimya kinafuata, watu wabaki huku wamesimama.

Anayewekwa apige magoti mbele ya askofu, na akiwa amesimama huku amevaa kofia yake Askofu ainue mikono yake juu ya anayewekwa, aimbe au aseme sala ya kuweka wakfu.

Mwenyezi Mungu, uwe nasi, kwa uwezo wako. Wewe ni chanzo cha heshima yote, unampa kila mtu daraja lake, unampa kila mtu huduma yake. Wewe hubadiliki, bali unauangalia uumbaji wako wote na kuufanya upya kwa njia ya mwanao, Yesu Kristo Bwana wetu; Yeye ndiye neno lako, nguvu yako, na hekima yako. Unaona mbele mambo yote katika maongozi yako ya milele na kuwapatia mahitaji watu wa kila kizazi.

Unalifanya kanisa, mwili wa Kristo, kukua na kufikia kwenye kimo cha utimilifu kama hekalu jipya na kuu. Unalitajirisha kwa kila aina ya neema na kulikamilisha kwa tofauti ya viungo kuutumikia mwili wote kwa kielelezo cha ajabu cha umoja. Ulisimamisha

huduma tatu za ibada na utumishi kwa ajili ya utukufu wa jina lako.

Kama watumishi wa hema yako, uliwachagua wana wa Lawi na uliwapa baraka yako kama urithi wao wa milele. Katika siku za kwanza za kanisa lako chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, Mitume wa Mwana wako waliweka watu saba wenye sifa njema kuwasaidia katika huduma ya kila siku ili kwamba mitume wawe huru zaidi kwa ajili ya maombi na kuhubiri. Kwa njia ya maombi na kuwekea mikono, mitume waliwakabidhi watu wale waliochaguliwa huduma ya kuhudumia mezani.

Askofu amwekee mikono yule anayewekwa huku akisema:

Kwa hiyo, Baba, kwa Yesu Kristo mwana wako, mpe Roho wako mtakatifu, mjaze neema yako na nguvu, na umfanye shemasi katika kanisa lako.

Askofu aendelee:

Bwana, mtazame mtumishi wako kwa upendo ambaye sasa tunamweka katika huduma ya ushemasi, kuhudumia katika madhabahu yako takatifu.

Bwana, umtume Roho wako Mtakatifu ili aweze kutiwa nguvu kwa kipawa cha karama zako saba za neema kuibeba kazi ya huduma kwa uaminifu.

Aweze kuzidi katika kila wema: katika upendo wa kweli; katika kuwajali wagonjwa na maskini, katika mamlaka ya unyenyekevu, katika kujirudi, na katika utakatifu wa maisha.

Katika mwenendo wake awe mfano katika amri zako na kuwaongoza watu wako kuiga mfano wa usafi wa maisha yake. Aweze kudumu katika kuwa na nguvu na kuwa thabiti katika Kristo, akiupatia ulimwengu ushuhuda wa dhamiri safi. Katika maisha haya aweze kumwiga mwanao, aliyekuja, si kutumikiwa bali kutumika, na siku moja amiliki pamoja naye mbinguni.

Tunaomba haya kupitia Bwana wetu Yesu Kristo, mwanao aishiye na kumiliki pamoja nawe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja, milele na milele. Amina.

Kukabidhi stole (na Dalmatic)

Baada ya sala ya kuweka wakfu, askofu huku akiwa amevaa kofia yake akae, na wanaowekwa wasimame. Baadhi ya mashemasi wasaidizi (au makasisi) wawavalishe stole ya ushemasi wale wanaowekwa.

Kupewa kitabu cha Injili

Huku akiwa amevaa kishemasi, anayewekwa aende kwa askofu na kupiga magoti mbele yake. Askofu ampe kitabu cha Injili huku akisema:

Pokea injili ya Kristo ambaye umekuwa mjumbe wake. Amini kile unachokisoma, fundisha kile unachokiamini. Na utendee kazi kile unachokifundisha.

Baada ya shemasi kupokea kitabu cha Injili, asimame. Ndipo askofu amlete mbele ya watu wote.

Kuweka wakfu Makasisi

Askofu bila kuwa na kofia (mitre) yake awaalike watu kuomba.

Watu wangu wapendwa, tuombe kwamba Baba mwenye nguvu zote awaminie watumishi wake hawa karama za mbinguni, ambao amewachagua kuwa makasisi.

Wote wapige magoti na kwa kimya kimya wawaombee wanaowekwa. Askofu huku akiwa amevaa kofia yake asimame na kusema:

Utusikie Bwana Mungu wetu, na uwamiminie watumishi wako hawa baraka ya Roho Mtakatifu na neema na nguvu ya ukuhani.

Tunawaleta mbele zako watu hawa wawekwe mikono; wategemeze kwa upendo wako usio na kikomo. Tunaomba haya kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

Wengine wote wasimame isipokuwa wanaowekwa wabaki wamepiga magoti mbele ya askofu. Askofu ainue mikono yake juu ya wanaowekwa halafu aanzishe sala ya kuweka wakfu:

Njoo utusaidie, Bwana, Baba Mtakatifu, Mungu Mwenyezi na wa milele; wewe ni chanzo cha kila heshima na ukuu wa maendeleo yote na uthabiti. Unaiangalia familia inayokua ya mwanadamu kwa karama yako ya hekima na kwa namna yako ya kuweka daraja. Ulipokuwa umekwisha kuwaweka makuhani wakuu kutawala watu wako, ulichagua watu wengine na kuwaingiza katika daraja na heshima ili wawe pamoja nao na kuwasaidia katika kazi zao; na hapo ndipo yalianzia madaraja ya makuhani na huduma ya walawi, na kuanzisha taratibu takatifu za ibada.

Kule jangwani uligawia roho ya Musa kwa watu sabini wenye hekima ambao walimsaidia kutawala kundi kubwa la watu wake.Ulishirikisha miongoni mwa wana wa Haruni Utimilifu wa nguvu za baba zao,kutoka makuhani wastahilio kwa idadi timilifu kwa ajili ya taratibu za ibada iliyokuwa ikiongezeka kwa kutoa dhabihu na ibada. Vivyo hivyo kwa utunzaji wako wa upendo uliwapa mitume wa mwana wako watu wa kuwasaidia katika kuwafundisha imani; Walihubiri Injili ulimwenguni kote.

Bwana,tujalie watenda kazi kama hao, maana sisi tu dhaifu na hitaji letu ni kubwa.

Makasisi wa CEC waliopo huku wakiwa wamevaa alb na Stole wapite mbele.

Askofu aweke mikono yake juu ya kichwa cha kila anayewekwa.kwa kuombwa na askofu,Makasisi wa CEC wanaweza kila mmoja kuweka mikono juu ya wanaowekwa .Baada ya kuwekwa mikono Makasisi wabaki pamoja na askofu hadi sala ya kuweka wakfu imemalizika.

Askofu peke yake aseme sala ya kuweka wakfu kwa mmoja mmoja. Atakayewekwa wakfu.

Kwa hiyo Ee baba kwa ajili ya Yesu Kristo Mwanao, Mpe Roho Mtakatifu huyu_____mjaze Neema na nguvu na kumfanya kasisi katika kanisa lako.

Askofu aombe sala ifuatayo ya kuweka wakfu kwa kila anayewekwa Mikono

Baba mwenyezi, wajalie watumishi wako hawa heshima ya ukuhani. Fanya upya ndani yao roho ya utakatifu.
Kama watenda kazi pamoja na daraja la maaskofu waweze kuwa waaminifu katika huduma ambayo wanapokea toka kwako, Bwana Mungu na wawe kielelezo cha mwenendo safi kwa wengine.
Waweze kuwa waaminifu katika kutenda kazi pamoja na daraja la maaskofu, ili kwamba maneno ya injili yafikie hadi mwisho wa nchi, na jamii ya mataifa wafanywe mmoja katika kristo,waweze kuwa watu watakatifu wa Mungu.Tunaomba haya kwa njia ya Yesu Kristo, Mwana wako, aishiye na kumiliki pamoja nawe na Roho mtakatifu, Mungu mmoja milele na milele . Amina.

Hapa kinafuata kipindi cha kuomba katika Roho kwa ajili ya makasisi wapya.

KUBARIKI MAVAZI.

Watu wanaweza kukaa.

Baada ya sala ya kuweka wakfu askofu, huku akiwa amevaa kofia yake akae na wale wanaowekwa wasimame .Stole na Chasuble kwa ajili ya wanaowekwa ziletwe kwa askofu , ambaye kwa kusaidiana na makasisi wake wazibariki kwa sala ifuatayo:-

Askofu : Msaada wetu u katika jina la Bwana
Watu: Aliyeziumba mbigu na nchi
Askofu: Bwana awe nanyi
Watu: Awe na roho yako.
Askofu: Na tuombe.

Mungu wa milele na mwenyezi, ambaye kupitia mtumishi wako Musa uliamuru mavazi yatengenezwekwa ajili ya kuhani mkuu,makuhani, na walawi ili wavikwe nakutenda kazi katika huduma yao mbele yako kwa heshima na utukufu wa jina lako.

Uwe karibu nasi tunaokuita na ubariki na utakase✝mavazi haya ya kikasisi kwa baraka yako yenye uwezo,kwa kuyamiminia neema yako toka juu,ili kwamba yawe ya kufaa nakuadhimisha kwa ajili ya ibada ya Kiungu na siri zako takatifu: na ujalie kwamba yeyote wa maaskofu wako,makasisi au mashemasi atakayevaa aweze kuhesabiwa kustahili kuokolewa na kulindwa dhidi ya magomvi na majaribu: Ujalie kwamba yatumike kwa usahihi na istahilivyo katika kuhudumia sacramenti zako takatifu mara kwa mara, na ziweze kudumu katika huduma yako kwa utulivu wakiungu.Kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

Askofu anaweza kuyanyunyizia mavazi kwa kutumia maji matakatifu. Awape Stole makasisi wanaowekwa.

Kubariki Stole Na Chasuble

Makasisi wa CEC warudi mahali pao.Askofu awape Makasisi wanao wasaidia mavazi,wapange stole kwa ajili ya wanaowekwa jinsi zitakavyovaliwa na makasisi na Wawavishe Chasuble.Mara wakisha kuvaa, Makasisi wanaowekwa warudi na kupiga magoti mbele ya askofu.

Kupaka Mikono Mafuta

Askofu apokee kitambaa cha kitani na Krisma, apake mafuta kidole gumba na kwenye kidole cha shahada cha kila mkono, achore alama ya msalaba kwenye viganja vya wanaowekwa huku wakiwa wamepiga magoti mbele yake.Askofu amwombee kila mmoja wakati wa kupaka mafuta mikono yao.

ASKOFU: Baba alimtia mafuta Bwana wetu Kristo kwa ajili ya nguvu za Roho Mtakatifu. Yesu na akuhifadhi kuwatakasa watu wa kristo na kutoa dhabihu kwa Mungu .

Mikono hii imetiwa mafuta kwa ajili ya huduma ya Mungu Mwenyezi -wewe ni kuhani milele mfano wa Melkizedeki.

Baada ya makasisi wanaowekwa kuwa wametiwa mafuta,watu wanaweza kusimama na kuimba huku askofu na makasisi waliowekwa wakinawa mikono yao.

Watu wamaweza kuketi .

Utoaji Wa Zawadi

Askofu ampe kila kasisi Biblia huku akisema.

ASKOFU : Pokea Biblia hii kama ishara ya mamlaka na majukumu uliyopewa kuhubiri neno la Mungu, Kutangaza kweli ya Mungu,na kuwa Mtu wa maombi.

Mashemasi waandae mkate katika sahani ya Ushirika na divai katika kikombe kwa ajili ya ushirika Mtakatifu,Walete sahani na kikombe kwa askofu ambaye huwapa makasisi wanaowekwa huku wakiwa wamepiga magoti.

ASKOFU: Pokea kutoka kwa watu wa Mungu zawadi zinazotolewa kwake kama dhabihu takatifu.
Ni ishara ya wito wako kama kasisi, uhudumu kwa uaminifu sacramenti zote takatifu.

Makasisi wanaowekwa warudishe sahani na kikombe kwa mashemasi ambao huviweka juu ya meza kwa ajili ya maandalizi ya ushirika Mtakatifu.Makasisi wanaowekwa watoe baraka kwa askofu.

Askofu awaite wake za makasisi wanaowekwa, na kuwaombea pamoja na familia zao. Ndipo awalete mbele ya watu.

Amani.

Askofu awasalimu makasisiwaliowekwa,ambao nao wawasalimu ndugu wa familia na wengine kama itafaa. Wachungaji na watu wasalimiane kila mtu na mwenzake kwa amani ya Bwana.

Ushirika Mtakatifu.

Shemasi aliyewekwa hutumika kama shemasi anayeanza,ataanzia huduma yake hapa. Anapaswa kuandaa meza, kusaidia mwenendo wa Ibada,kuhudumu kikombe wakati wa ushirika Mtakatifu, kutoa ghofira, na kuwaaga watu.

Matoleo

Neno la Maandiko:
" Mkaenende katika upendo,kama Kristo naye alivyowapenda ninyi,tena akajitoa kwa ajili yetu,sadaka na dhabihu kwa Mungu,kuwa harufu ya manukato" (Waefeso 5:2).
Askofu aondoe Cope yake na kofia na kuvaa chasuble kwa ajili ya kuadhimisha ushirika Mtakatifu.

Wimbo Waweza Kuimbwa Wakati Wa Matoleo.

Mhudumu ainue chombo cha matoleo yaliyotolewa,Mkate,divai kwa zamu,na aseme sala zifuatazo:-

Mhudumu: Ubarikiwe ewe Mungu baba wa maumbile yote,
Katika wema wako tunayo haya mafungu pamoja na sadaka ambayo ni ishara ya maisha na kazi zetu; na vitumike katika kanisa lako kwa kazi uliyoiweka mbele yetu na kwa kuendelea ufalme wako.

Waumini: Ubarikiwe Mungu Milele.

Mhudumu: Ubarikiwe wewe, Bwana Mungu wa viumbe vyote.
Tunakutolea mkate huu kwa ajili ya wema wako. Zao la dunia hii na kazi ya mikono yetu;
Mkate huu uwe kwetu mwili wa Kristo.

Waumini: **Ubarikiwe Mungu Milele**

Mhudumu:Wewe Bwana Mungu wetu,tunapochanganya maji na divai hii ni kito cha ushirika wa uungu na asili ya kibinadamu ya Yesu Kristo,tunaonywea kikombe hiki na

tushiriki katika uungu wa Kristo ambaye yeye mwenyewe alijinyenyekeza kushiriki katika ubinadamu wetu.

Waumini: **Amina**

Mhudumu:Ubarikiwe wewe,Bwana Mungu wa viumbe vyote. Kwa ajili ya wema wako tunakutolea divai hii,tunda la mzabibu Na kazi ya mikono yetu binadamu; divai hii iwe kwetu damu ya Kristo.

Waumini: Ubarikiwe Mungu Milele

Mhudumu : Natuombe,ndugu zangu,ili sadaka yetu iweze kupokelewakwa Mungu,Baba mwenyezi.

Waumini: Mungu na apokee sadaka hii iliyo katika mikono yako kwa ajili ya sifa na utukufu wa jina lake, kwa ajili ya mema juu yetu na wema wa kanisa lake lote.

Wimbo wa Sifa (Doxology)

Msifuni Mungu ambaye toka kwake baraka zote hububujika .
Msifuni yeye Viumbe vyote hapa chini.
Haleluya,Haleluya.
Msifuni juu,enyi wenyeji wa mbinguni.
Msifuni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.
Haleluya, Haleluya,Haleluya,Haleluya Haleluya.

SHUKRANI KUU

Watu wabaki wamesimama na mhudumu awaelekee na kusema:

Mhudumu: Bwana awe nanyi
Waumini : **Awe pia na roho yako**
Mhudumu: Inueni mioyo yenu
Waumini: **Twaiinua kwa Bwana**
Mhudumu: Na tumshukuru Bwana Mungu wetu
Waumini: **Ni haki kumshukuru na kumtukuza**

Mhudumu aendelee na maneno haya:

Ni jambo la haki,jema na la furaha kuu,wakati wote na
Kila mahali kumshukuru Mungu,Baba mwenyezi muumba wa mbingu na nchi.

Kupitia Mchungaji mkuu wa kundi lako Yesu Kristo Bwana wetu,ambaye baada ya kufufuka kwake aliwatuma mitume wake waende kuhubiri na kuwafundisha mataifa yote; na aliahidi kuwa pamoja nao hadi utimilifu wa dahari.

Kwa hiyo,tunakusifu wewe,tukiunganisha sauti zetu na malaika,na makerubi pamoja na jeshi lote la mbinguni ambao milele huimba wimbo huu wa kutangaza utukufu wa jina lako.

Mtakatifu Wa Watakatifu.

Mtakatifu, Mtakatifu,Mtakatifu Bwana ,Mungu mwenye nguvu na mwenyezi, Mbingu na nchi zimejaa utukufu wako.
Hosana palipo juu.
Abarikiwe yeye ajaye katika jina la Bwana.
Hosana palipo juu.

Waumini wasimame au wapige magoti.Mhudumu aendelee:

Bwana Mtakatifu na mwenye Rehema:Kwa upendo wako usio na kikomo ulituumba kwa ajili yako,na tulipokuwa tumeanguka katika dhambi na kuwa watumwa wa dhambi na mauti,wewe kwa huruma yako ulimteta Yesu Kristo, mwana pekee wa milele kushiriki asili yetu ya ubinadamu,kuishi na kufa kama mmoja wetu,Kutupatanisha na wewe Mungu,Baba wa wote.Alitandaza mikono yake msalabani ,na kujitoa mwenyewe, kwa kutii mapenzi yako, sadaka kamili kwa dunia yote.

Katika maneno yafuatayo, mhudumu ashikilie au aweke mikono juu yake;na kwa maneno yahusuyo na kikombe; ashikilie au kuweka mkono juu ya kikombe na viriba vinginevyo vyenye divai kwa ajili ya wakfu.

Na kwa hiyo, Baba, ambao tumeokolewa naye na kufanywa viumbe wapya kwa maji na kwa Roho Mtakatifu,sasa tunakuletea zawadi hizi. Zitakase✝kwa Roho wako mtakatifu ziwe mwili na damu ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Yeye usiku ule aliotolewa kwa mateso na kifo, Bwana wetu Yesu Kristo alitwaa mkate; na akiisha kukushukuru,aliumega na akawapa wanafunzi wake akisema " Twaeni mle: Huu ndio mwili wangu, uliotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi".

Baada ya chakula alitwaa kikombe cha divai; na alipokuwa ameshukuru, aliwapa wanafunzi wake akisema,"Nyweeni katika hiki ninyi nyote: Hii ni damu yangu ya agano jipya,ambayo imemwagika kwa ajili yenu na kwa wengi kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Fanyeni hivi kila mnywapo kwa kunikumbuka mimi"

Kwahiyo tunatangaza maajabu ya Imani.

Mhudumu Wa Waumini.

Kristo Amekufa
Kristo Amefufuka
Kristo atakuja tena.

Mhudumu anaendelea
Tunashangilia kumbukumbu la wokovuwetu,Ee Baba,kwa sadaka na shukrani.Tukikumbuka kifo chake,ufufuo na kupaa kwake,tunatoa zawadi hizi.✝ Zitakase kwa Roho wako mtakatifu Ili kwa watu wako ziwe mwili na damu ya mwanao Yesu,Chakula kitakatifu,kinywaji kipya na maisha yasiyo na kikomo kwake. Tutakase pia ili kwa uaminifu tuweze kupokea sakramenti yako takatifu, na tukutumikie katika umoja,Kiasi na amani; na siku ya mwisho utulete pamoja na watakatifu wako katika furaha ya ufalme wa mbinguni.Tunaomba haya yote kupitia jina la mwanao YesuKristo:Kwa yeye na katika yeye na ndani ya yeye kwa umoja wa Roho Mtakatifu heshima na utukufu ni wako, Baba mwenyezi,sasa na hata milele Amina.

SALA YA BWANA

Na sasa kama mwokozi Yesu Kristo alivyotufundisha,tunathubutu kusema.

Waumini na Mhudumu.
Baba yetu uliye mbinguni,jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe,hapa duniani Kama huko mbinguni, utupe leo Mkate wetu wa kila siku Na utusamehe makosa yetu, kama nasi tunavyowasamehe waliotukosea .Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.Kwa kuwa ufalme ni wako,na nguvu, na utukufu, hata milele.Amina.

Kuumega Mkate.

Mhudumu anamega mkate uliowekwa wakfu
Hapa kunakuwa na kipindi cha ukimya.Halafu aseme:
Mhudumu: (haleluya) Kristo pasaka wetu amekwisha kutolewa kwetu; kwa hiyo na tusherehekee karamu yetu (Haleluya)

Halafu panaweza kuimbwa au Kusemwa:

Mwanakondoo wa MunguUchukuaye dhambi za ulimwengu;
Uturehemu.
Mwanakondoo wa Mungu Uchukue dhambi za ulimwengu;
Uturehemu.
Mwanakondoo wa Mungu Uchukuae dhambi za ulimwengu;
Utupe amani yako.

Tazama mwanakondoo wa Mungu; Mtazame yeye achukuaye dhambi ya ulimwengu. Heri walioalikwa kwenye karamu ya mwanakondoo.
Bwana, Sistahili kukukaribisha,lakini sema neno tu nami nitakuwa mzima.

Akiwaelekea watu, mhudumu awakaribishe waumini ifuatavyo:-

Zawadi ya Mungu kwa watu wa Mungu.

Pia anaweza kuongeza.

mtwae kwa kumbukumbu kuwa Kristo alikufa kwa ajili yenu,mleni Yeye mioyoni mwenu kwa shukrani.

Wahudumu wanapokea sakramenti kwa namna zote na mara moja wanatoa kwa waumini.

Mkate na kikombe vinatolewa kwa washiriki kwa maneno haya:
Mwili (damu) ya Bwana wetuYesu Kristo ikulinde hata uzima wa milele.(Amina)

Au kwa maneno haya:-

Mwili wa Kristo Mkate wa Mbinguni.(Amina).
Damu ya Kristo, kikombe cha wokovu. (Amina).

Wakati wa huduma ya ushirika mtakatifu, nyimbo, zaburi,au nyimbo za utaifa zinaweza kuimbwa.

Wakristo wote waliobatizwa katika Jina la Baba na Mwana na Roho mtakatifu,na wanaokubali uwepo wa kweli wa Yesu katika Sakramenti,na wanaoruhusiwa kupokea ushirika mtakatifu katika kanisa lao, wanakaribishwa kupokea mwili na damu ya Yesu Kristo.

Sala baada ya Ushirika kwa ajili ya wanaowekwa.
Baada ya ushirika mhudumu aseme:

Na tuombe.
Wote wapige magoti Askofu na watu(pamoja) waliowekwa wakae kimya.

Baba Mwenyezi twakushukuru kwa kutulisha chakula kitakatifu cha
Mwili na damu ya Mwanao, na kwa kutuunganisha kwa njia yake katika ushirika wa Roho wako mtakatifu.
Tunakushukuru kwa kuinua watumishi waaminifu toka miongoni mwetu kwa ajili ya huduma ya neno lako na sakramenti zako.
Tunaomba kwamba shemasi huyu ambaye ni wako aweze kutufaa akiwa mfano katika maneno na matendo,katika upendo na uvumilivu na katika utakatifu wa maisha . Tujulie kwamba

sisi,pamoja naye, sasa tuweze kukutumikia wewe na kufurahia daima katika utukufu wako, kwa njia ya Yesu Kristo mwana wako, Bwana wetu, aishiye na kumiliki pamoja nawe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja,sasa na hata milele.Amina.

Baraka

Mungu aliyeanzisha kanisa lake juu ya mitume akubariki kupitia Maombi ya watakatifu. **Amina**.

Mungu na akutie moyo kufuata mfano wa Mitume na kuishuhudia kweli kwa watu wote. **Amina**.

Mafundisho ya mitume yameimarisha imani yako .
Maombi yao yaweze kukuongoza kwenye kweli na makao ya milele.
Amina.

Mungu mwenyezi akubariki, ✝Baba,Mwana na Roho Mtakatifu.
Amina.

Wimbo.

Kuwaaga Watu.

Shemasi awaage watu kwa maneno haya:
Haleluya, Haleluya! Tuenendeni Ulimwenguni; tukifurahia katika nguvu za Roho Mtakatifu.
Shukrani ziwe kwa Mungu Haleluya.

Mwisho.